**JAMHURI YA RWANDA**

**WIZARA YAELIMU**
**TAASISI YATAIFA YA UKUZAJI MITAALA**
**S.L.P 608 KIGALI**

# MUHTASARI WA SOMO LA KISWAHILI

## KIDATO CHA IV, V, NA VI

**2007**

## Utangulizi

Kiswahili ni lugha ambayo inazungumzwa  na watu wengi  tena wenye fani mbalimbali Ulimwenguni .
Lugha hii  yenye asili ya kibantu imeshapiga hatua  kimatumizi,  kisarufi na kimsamiati pia  Kiswahili  ni lugha yenye  asili ya mwambao wa pwani ya Afrika  ya mashariki yenye lahaja  mbalimbali  inayotumiwa na watu  wengi  wa Afrika  ya Mashariki na kati na ulimwengu kwa jumla.

Jamii ya Wanyarwanda imezungukwa na jamii nyingi ne zinazozungumza lugha hii.Kutokana  na hali hii inahitaji  mawasiliano katika fani mbalimbali  ili  kukabiliana  vizuri  na ulimwengu  wa sayansi na tekinolojia

.Mhutasari huu unawalenga wanafunzi wa mkondo wa lugha kwa miaka mitatu, yaani kidato cha nne,tano na sita ikiwa ndiyo wanaanza kabisa kujifunza lugha ya Kiswahili.

Hii imetokana na marekebisho yaliyofanywa ili kuleta uoanishaji wa mitaala inayofaa jamii ya Wanyarwanda .

Ili kumsaidia mwalimu kufundisha vizuri zaidi somo la Kiswahili , mhutasari huu umegawanywa ki vitato, kwa kila kidato kidato zimependekezwa mada zitakazofundishwa .Pia , vitabu vya kiada kwa mwalimu na mwanafunzi vimeonyeshwa kwavidato vyote. Vile vile malengo ya jumla , malengo mahsusi, njia za kufundishia na kujifunzia , Tathmini na vitabu vya rejea vimeonyeshwa .

Jambo la muhimu ni kwamba ,njia zilizowekwa katika mhutasari huu ni mapendekezo tu . Mwalimu anatazamiwa kutumia ujuzi wa ubunifu wake katika kutumia njia nyingine mbailimbali, vifaa pamoja na vitabu vya ziada .

**MWONGOZO**

Lugha ya Kiswahili kama tulivyosema katika utangulizi ni lugha iliyo na asili ya kibantu ambayo Kinyarwanda ni mojawapo ya lugha hizo.Kwa maana hiyo lugha hii tunatarajia haitakuwa ngumu au ngeni sana katika masikio ya Wanafunzi Wanaokusudia kujifunza lugha hii , mathalani katika Kiswahili maneno mengine yana tofauti ndogo nay ale ya kinyarwanda au yamekopa namna moja kutoka nje.

| kiswahili | kinyarwanda |
|---|---|
| shati | ishati |
| karatasi | ikaratasi |
| koti | ikoti |
| barua | ibaruwa |
| mtu | umuntu |
| mbwa | imbwa |
| sahani | isahani |

Kwa hiyo kuna upatanisho wa ki-sarufi ambao hauko mbali sana na wa Kinyarwanda .

Mwongozo huu pia umelenga kwenye matakwa na mahitaji ya nchi yetu katika kumjenga Mwanafunzi ili aweze kuisaidia jamii katika kukabiliana na matatizo mbali mbali , kwa mfano kujilinda na magonjwa yanayotokana na zinaa na hasa ukimwi.

Lugha hii , itamsaidia mwanafunzi kupanua mawazo yake katika kuwasiliana na watu wengine kutoka jamii mbali mbali hivyo kuelewa maisha ,utamaduni na mambo mbali mbali yanayoweza kumsaidia yeye na jamii kwa ujumla , hivyo kumjengea tabia ya kuwa na heshima , uvumilivu ,upendo ,amani, haki , umoja na mshikamano pia demokrasia .Vili vile ataweza kujenga tabia ya kujiamini, kuwa huru katika kutoa mawazo yake hivyo kutambua kuwa ana wajibu wa kuheshimu haki za binadamu na kuzingatia utu wa mtu .Mwanafunzi huyu pia anatarajiwa kuwa na mawazo ya kuondokana na ubaguzi wa aina yoyote , uwe wa
Ki-kabila ,Ki- dini , Kijinsia n.k.
Ni matumaini yetu kuwa haya yote yatazingatiwa katika mhutasari huu.

Mwalimu anashauriwa kuchunguza yale ambayo yanafanana katika lugha mbili ili aweze kuyafundisha kwa urahisi.

Ili afikie malengo makuu ya mhutasari, mwalimu anashauriwa kuzingatia malengo hayo kila anapofundisha ili asifundishe mengine na akakosea shabaha zake.

Mwalimu anashauriwa kujaribu njia ya kufundisha lugha za kigeni ijulikanayo kwa jina la
( Audio Lingual Method). Mojawapo ya mambo njia hiyo inasisitiza ili kusaidia muhtasari kufikia malengo yake ni kufundisha hapa na pale miundo ambayo wanafunzi wanahitaji kwa kuwasiliana au kuelewa vifungu wanavyotakiwa kusoma.

Mwalimu anatakiwa kufundisha miundo kutokana na na hali halisi yamatumizi yake kama vile mazungumzo katika vinasa sauti, nyimbo n.k.Hivyo polepole miundo hiyo itajulikana bila kuonekana kuwa ilikuzsudiwa kufundishwa mahali ambapo haikutayarishwa kwenye mhutasari.

Audio Lingual Method inasisitiza kuwa kufundisha lugha ni kuzingatia mazingira kwa ujumla .

Ikiwa mwalimu ameamua kufundisha msamiati wa vitenzi,mifano itakayotolewa itakuwa ni yenye mada hizo yaani uhusiano nayo ,majina na mambomengine yatakuwa na mwelekeo huo.

Mara nyingi mwalimu ataanza somo lake kwa kutoa kifungu chenye mazungumzo au hadithi ili kudhihirisha hali halisi ya matumizi ya mambo anayotaka kufundisha.

Kifungu kitasomwa kikiwa kifupi sana ,wanafunzi wataombwa kukikariri.

Hali hiyo ya kufundisha mambo yenye kuhusu mazingira Fulani katika somo inasaidia wanafunzi kufikiria wenyewe maana ya maneno mengine kwa sababu yanakwenda pamoja.

**MADHUMUNI YA JUMLA KATIKA UFUNDISHAJI WA LUGHA YA KISWAHILI**:

1. Kumjengea Mwalimu msingi bora wa kutumia lugha hii na kuweza kuendelea na elimu ya juu

2. Kumpa mwanafunzi uwezo wa kutumia lugha ya Kiswahili katika shughuli mbali mbali za Kitaifa na Kimataifa .

3. Kumtayarisha mwanafunzi ili awe mjenzi bora wa lugha ya Kiswahili

4. Kusaidia kukuza uwezo wa mwanafunzi katika kuongea lugha hii na kuweza kuitumia muda wote katika shughuli za ujenzi wa taifa

5. Kukuza uwezo wa Mwanafunzi katika kujisomea na kuelewa mambo mbali mbali yaliyomo katika lugha ya Kiswahili.

6. Kumsaidia mwanafunzi afikiri ajitegemee katika mawazo yake, aweze kubuni na awe msanifu hodari.

7. Kumwezesha mwanafunzi kusoma upesi na kuwlewa anachokisoma .

8. Kumwezesha mwanafunzi kutumia mitindo mbalimbali katika kuzungumza na kuandika .
9. Kujenga tabia ya utafiti na udadisi katika kiswahili na katika maisha kwa ujumla .

**KIDATOCHA NNE**

| MADA KUU | MADA NDOGO | MADHUMUNI MAHUSUSI |
|---|---|---|
| **1. MAAMKIZI**<br><br><br><br><br><br><br><br><br><br>**NAFSI** | 1.Maamkizi Darasani<br>2.Maamkizi nyumbani<br>3.Maamkizi kwa watu wazima<br>4.Maamkizi kwa watu wa rika moja<br>5.Kuaga<br>6.Aina ya maamkizi<br>7.Aina ya maamkizi<br><br>Msamiati uhusiano wa familia | -Mwanafunzi aweze kutofautisha Salamu mbali mbali kulingana na mazingira au nyakati.<br><br>-Mwalimu aweze kutumia Salamu hizo kulingana na rika mbali mbali . |

| | | |
|---|---|---|
| | Umoja na Wingi<br><br>Umoja Uwingi<br><br>Mimi Sisi<br><br>Wewe Ninyi nyie<br><br>Yeye Wao | -Mwalimu aweze:<br><br>1.Kutumia nafsi mbali mbali katika Mazungumzo<br><br>2.Kutofautisha matumizi ya nafsi. |
| | Matumizi Nafsi katika Mazungumzo<br>Mfano :<br>a)Mwalimu na Mwanafunzi | |

| | | |
|---|---|---|
| **2.ALFABETI** | b) Mwanafunzi Mwanafunzi<br><br>i) irabu ( a,e,i,o,u,)<br><br>ii) konsonanti( b, d h,f n.k<br><br>iii) Matamshi yanayotokana na mfuatano wa vitamkwa<br><br>mfano -mbw-a<br>-mf- u<br>- ua- | Mwanafunzi aweze:<br><br>Kutumia irabu na konsonanti katika kuunda maneno<br><br>Kutamka kwa lafudhi sanifu ya Kiswahili<br><br>Kutambua irabu na konsonanti katika neno. |
| | | |

| | | |
|---|---|---|
| **3.MSAMIATI** | i) Uhusiano wa familia kama : BabMama , Mjomba ,Shangazi, Kaka,Dada, Mpwa n.k<br><br>ii) Dira , Saa,Majina ya Miezi , ya Miakana Misimu Kuhesabu.<br><br>iii) Magonjwa<br>Mfano :Ukimwi(sida) , malaria ,homa , uti wa mgongo, kuhara , mafua n.k<br><br>iv) Rangi mbalimbali<br><br>v) Wanyama wafugwao,wa porini , wa mjini ndege wafugwao, na wasiofugwa na | 1.Mwanafunzi aweze :<br><br>-Kutumia msamiati<br><br>2.Aweze kutoa maana ya msamiati<br><br>3. Aweze kuonyesha uhusiano na<br>Utofauti wa mambo yajengayo familia<br><br>4.Aweze kujua majira , sehemu za mwili<br><br>Maumbo mbalimbali ,, wanyama na rangi<br>mbalimbali na baadhi ya magonjwa ya |

| | | |
|---|---|---|
| **4. MATUMIZI YA NYAKATI** | wadudu .<br><br>vi Sehemu za mwili<br><br>vii Maumbo mbalimbali mfano :Pembetatu,mraba,mstatili,duara n.k<br><br>viii) Tarakimu<br>ix) Kazi za ufundi mbali mbali.<br>x) msamiati wa mazingira tofauti<br>mfano darasani nyumbani sokoni n.k<br><br>i) Dhana yaWakati katika Kiswahili ( hali yakinishi) | Kawaida .<br><br>Mwanafunzi aweze<br>1.kutumia msamiati<br>2.kutoa maana ya misamiati iliyotumika<br><br>1.Mwanafunzi aweze kutumia nyakati Mbalimbali katika |

| | | |
|---|---|---|
| | a) <u>Wakati uliopo : -NA</u><br><br>Mfano i) Mtoto anakula<br>ii) Kalisa anacheza<br><br>b) Wakati ujao :-TA<br><br>i) Mwalimu atafundisha Kiswahili kesho<br><br>ii)Mutesi atafika kesho<br><br>c) Wakati uliopo-LI<br><br>Mfano<br>i)Mwalimu alifundisha | mazungumzo.<br><br>2.Mwanafunzi aweze kutumia nyakati tofauti katika mazungumzo na maandishi.<br><br>3.Mwanafunzi aweze kujifunza nyakati za kawaida na rahisi kuelewa maana ndipo anapoanza kujifunza Kiswahili. |

| | | |
|---|---|---|
| | Kiswahili<br><br>ii)Kirenga alikimbia<br><br>d) Wakati wa mazoea HU<br><br>Mfano<br>i)watoto hulia ovyo ovyo kila siku<br>ii)wanafunzi hucheza mpira vizuri.<br><br><br>e)Wakati uliotimilika-ME-<br>Mfano:<br>-Mimi nimelima shamba<br>-Wao wamekimbia sokoni | |

| | | |
|---|---|---|
| **5. HALI YA KUKANUSHA NA KUYAKINISHA** | ii)Dhana ya wakati katika hali ya kukanusha<br><br>a) Wakati uliopo<br>mfano :<br>mtoto hali chakula<br>.<br>mtoto hachezi.<br><br>b)Wakati ujao<br>Mfano:<br>-mwalimu hafundishi kesho<br>- Mutesi hatafika shuleni.<br><br>c) Wakati uliopita<br>mfano:<br>Mwalimu hakufundisha Kiswahili jana | Mwanafunzi aweze kutunga<br><br>sentensi za nyakati mbali mbali kwenye hali ya kukanusha , na kuyakinisha . |

| | | |
|---|---|---|
| | -Yohana hakufika shuleni wiki iliyopita<br><br>d)Wakati wa mazoea<br>mfano:<br>-Watoto hawalii ovyo<br><br>-wanafunzi hawachezi mpira asubuhi<br><br>e)Wakati uliotimilika<br>-Mimi sijalima shamba<br>-wao hawajaenda sokoni | |

| | | |
|---|---|---|
| **6.SARUFI MAUMBO**<br><br>**(AINA SABA ZA MANENO)** | 1.Jina / Nomino-N<br><br>- Maana ya Nomino/jina<br>Aina za nomino<br>-Majina/nomino ya pekee<br><br><br>Mfano –Majina ya watu<br>-mahali<br>-milima<br>-mito<br>-nchi<br>-maziwa<br><br>-Nomino /majina ya jumla<br>( makundi)<br>Mfano : nyumba ,askari,meza,shule n.k | Mwalimu aweze<br><br>1.Kueleza maana ya nomino au majina<br>1.<br>2.Kuonyesha/kubainisa aina za nomino na<br>na majina |

| | | |
|---|---|---|
| | -Nomino/majina ya dhahania ( maarifa)<br>Mfano :upepo,upole,ugonjwa, chafya,<br>Ukarimu,usingizi, n.k | |
| | 2. VIWAKILISHI( W)<br>Maana ya viwakilishi | Mwanafunzi aweze kuonyesha na kuainisha Viwakilishi<br>vya – kuonyesha<br>-kuuliza |

| | | |
|---|---|---|
| | 3.VIVUMISHI(V)<br>Maana ya vivumishi<br><br>aina ya vivumishi | Wanafunzi aweze kuonyesha na Kuainisha vivumishi vifuatavyo<br><br>Vivumishi – vya sifa au idadi<br><br>-kuonyesha<br>-kuuliza<br>-kumiliki<br>-majina<br>-a-unganifu<br>-enye –enyewe<br>-ote –ingine |
| | 4.VITENZI(T)<br>Maana ya kitenzi | Mwanafunzi aweze<br>1.Kuelewa- maana ya vitenzi na |

| | | |
|---|---|---|
| | Mfano wa vitenzi :<br>Kula, kulima, kucheza , kuimba<br>Aina za vitenzi<br>- Kitenzi kikuu (T)au(Ft)<br>Mfano : Mama <u>analima</u><br>- T<br>- Kitenzi kisaidizi TS au ( f Ts)<br>Mfano: <u>Kalisa</u> a<u>likuw</u>a <u>anasoma</u><br>T N TS<br>-Kitenzi kishirikishi t<br><br>Mfano:-Bizimana<u>ni</u> mpole<br>-Kagabo <u>ni </u>mrefu<br>t<br>-Uwamariya <u>si </u>mvivu<br>t<br>-Dada <u>si</u> mchoyo | - aina za vitenzi<br>2. Kutofautisha aina za vitenzi<br><br>3.Kutumia aina za vitenzi katika<br>Sentensi.<br><br><br><br><br>Mwanafunzi aweze<br>1. Kutunga sentensi kwa kutumia hali mbali mbali<br><br>2.Kubadili sentensi kutoka hali moja hadi nyingine |

| | | |
|---|---|---|
| | t<br><br>Hali ya Vitenzi<br><br>Matumizi ya vitenzi katika hali Mbalimbali<br><br>mfano :<br><br>a) Hali ya kueleza<br><br>mfano: Yohana analima shamba<br><br>b)Hali ya kuuliza<br>mfano:jeunakwenda shambani? | 3.kutambua hali ijengayo sentensi |

| | | |
|---|---|---|
| | c)Hali ya kuwa<br>mfano:Hii ni nyumba ndefu.<br><br>d) Hali ya kuomba<br>mfano:<br>tafadhalimwalimu ninaomba<br>Ruhusa ya kutoka nje<br><br>e) Hali ya kuamuru<br>mfano :toka nje | |

| | | |
|---|---|---|
| | | |
| | VIELEZI<br>Maana ya vielezi | Mwanafunzi aweze<br>Kuelewa maana na aina ya vielezi<br>Kuainisha vielezi katika tungo |

| | | |
|---|---|---|
| | VIUNGANISHI NAVIHISISHI<br><br>Maana ya viunganishi<br>Maana ya vihisishi | Mwanafunzi aweze<br>Kuelewa maana,aina na matumazi ya viunganishi na vihisishi |

| | | |
|---|---|---|
| **7. a)UFAHAMU**<br><br><br><br><br>**b)KUSOMA** | a-Kusoma hadithi na vifungu vya habari<br>b-Hadithi fupi fupi<br><br><br><br>Hadithi:<br>a)hadithi fupi fupi.<br><br>b)Vifungu vya habari | Mwanafunzi aweze<br>i) Kusimulia hadith aliyoisoma, Aliyosomewa,au aliyoyasoma.<br><br><br><br>Mwanafunzi aweze<br>Kusoma kwa kuzingatia lafudhi, shadda<br>Matamshi n.k<br><br>Kusoma upesi kwa kutafakari |

| | | |
|---|---|---|
| | | Aliyoyasoma |
| **8 .TUNGO** | i).Maana ya Tungo<br>ii Aina za tungo kwa misingi ya muundo<br><br>a) Tungo sahili<br>mfano -:Mutesi anaimba<br>-Mukantwari analima | Mwanafunzi aweze:<br>1.Kueleza maana ya tungo<br>2.kuainisha tungo<br>3.kutunga aina mbali mbali za tungo |

| | | |
|---|---|---|
| | b) <u>Tungo tegemezi/mseto</u><br>mfano:-atakapofika<br>-anapoimba<br>c)Tungo changamano<br>mfano:<br>d) Tungo ambatano<br>mfano:<br>-Ruhumuliza amekuja na anaimba<br>-Gatabazianalima na anabishana | |
| | | |

| | | |
|---|---|---|
| **9.VITUO NA ALAMA** | a)Matumizi ya:<br>-mkato (,)<br>-nukta (.)<br>-kuuliza (?)<br>-kushangaa ( )<br>-mtajo ( “ ”)<br>-nukta na mkaato (,, _ )<br>-nukta mblili (: )<br>-mabano ( )<br>- kistari kifupi ( __ )<br>- mstari wa mshazari ( )<br><br>b) matumizi ya herufi kubwa na ndogo | Mwanafunzi aweze Kutumia alama na vituo katika taaluma ya kusoma na kuandika |

| | | |
|---|---|---|
| **10.UTANGAJI** | Matumizi ya:<br><br>-Insha<br>-Barua za Kikazi<br>-Simu | Mwanafunzi aweze:<br>Kuandika insha , barua ya kirafiki<br>na simu kwa kufuata utaratibu<br>unaostahili.<br>Mwalimu aweze kutofautisha miundo ya<br>Tungo hizo. |

**KIDATO CHA TANO**

| MADAKUU | MADA NDOGO | MADHUMUNI MAHUSUSI<br>( mambo ya kuzingatia) |
|---|---|---|
| **1.SARUFI MAUMBO** | Muundo wa lugha<br><br>Aina za tungo kwa msingi wa maana<br><br>Tungosahili:<br>k.m John amefika<br><br>Tungo tegemezi :<br>k.m aliyefika | Mwanafunzi aweze<br><br>**i)**Kutaja na kutambua aina za tungo kwa msingiwa maana<br><br>ii)Kutofautisha tungo kwa msingi wa maana<br><br>iii)kutunga aina mbalimbali za tungo zenye maana<br>kwa kuzingatia maana<br><br>iv) Kutoa tungo nyingi zenye utata |

| | | |
|---|---|---|
| **2. UTUNGAJI** | Tungo nyofu<br>k.m sitaki kunywa maji<br>Tungo tata<br>k.m nyumbani kwetu kuna ua<br>utata ua -Ua , pambo<br>Ua ugo<br>Ua , msichana<br><br>i.Barua za kikazi<br>ii.Barua za kibiashara<br>iii. Barua za mialiko<br>iv Barua za gazetini | Mwanafunzi aweze<br><br>Kuandika barua kwa kufuata muundo wa taratibu za uandishi wa barua .<br><br>Kuandika barua mbali mbali |
| | | |

| | | |
|---|---|---|
| **3.MATUMIZI YA NYAKATI MBALI MBALI** | Mfano**:**<br><br>Ningelimuona ningelimwambia<br><br>Ningalimuona ningalimwambia<br>Alipomuona akashtuka<br>Atamkamata na kumfunga kamba | Mwanafunzi aweze<br>Kutumia nyakati mbalimbali katika tungo |
| **4.KUSOMAUFAHAMU NA MHUTASARI** | Vifungu vya ufahamu:<br>- msamiati<br>- kusoma<br>- ufupisho | Mwanafunzi aweze<br>- Kusoma vifungu vya habari mbalimbali<br>- kusoma kwa wepesi kusoma kwa makini<br>- kufupisha habari` |
| | | |

| | | |
|---|---|---|
| **5.NGELI ZA MAJINA** | Ngeli ya kwanza hadi ya nane<br>i)Ngeli ya kwanza A-WA<br><br>ii) Ngeli pili U-I<br>iii)Ngeli ya tatu KI-VI<br>iv) Ngeli ya nne LI---YA<br>v) Ngeli ya tano U<br>vi) Ngeli ya sita U-I-ZI<br>vii) Ngeli ya saba PA-M-KU<br>viii) Ngeli ya nane KU<br><br>mfano:<br>i)Mtoto analima / Watoto wanalima<br>ii)Mti umeanguka/ Miti imeanguka<br>iii)Kisu kimepotea/ Visu | Mwanafunzi aweze<br>Kutaja aina za ngeli mbalimbali<br>Kujua na kutumia ngeli mbalimbali |

| | | |
|---|---|---|
| | vimepotea<br>iv) Daftari limechanika/ Madaftari yamechanika<br><br>v) Upole umezidi<br><br>vi)Nyumba nzuri imejengwa/ nyumba nzuri zimejengwa<br><br>vii)Hospitalini kuna maajabu/ Hospitalinikunamaajabu<br>viii) Kucheza kumemchosha / kucheza kumewachosha | |
| | | |

| | | |
|---|---|---|
| **6.FASIHI SIMULIZI** | Tanzu za fasihi simulizi:<br>i)Methali<br>ii)Vitendawili<br>iii)Nahau<br>iv)Nyimbo<br>v)Ngonjera<br>vi)Tenzi<br>vii)Mashairi<br>viii)Majigambo<br>ix) Tamathari za semi | Mwanafunzi aweze<br>i)Kutaja tanzu za Fasihi Simuluizi<br><br>ii)Kutofautisha tanzu mbalimbali za fasihi simulizi<br><br>ii) Kutumia tanzu tanzu za fasihi kulingana na mazingira |
| **7 .MATUMIZI YA LUGHA YA KISWAHILI** | i) Rejesta za shughuli mbalimbali<br>mfanosoko, bungeni,shuleni ,jeshini n.k<br><br>iii) Mabadiliko katika | Mwanafunzi aweze:<br>i) Kutumia misamiati mbalimbali, kulingana na mazingira<br>ii) Kutofautisha maneno yenye maana zaidi ya moja |

| | | |
|---|---|---|
| | matumizi ya Kiswahili kulingana na mazingira na wakati<br>Mfano:-kunyonya<br>-beberu<br>- kupe<br>-ruzuku | |
| **8. USEMI WA ASILI NA USEMI ASILIA** | i) Usemi wa asili<br>- maana<br>-mifano mbalimbali<br>``utanikuta mjini jioni``<br>Juma alimwambia rafiki yake<br><br>ii) usemi wa taarifa<br>-Juma alimweleza rafiki yake kuwa angelimkuta mjini jioni ile n.k | Mwanafunzi aweze<br>-Kujua maana ya usemi asili na taarifa<br>-Kutofautisha usemi wa asili na taarifa . |

| | | |
|---|---|---|
| | | |
| **9.HISTORIA YA KISWAHILI** | **i**)Chimbuko la Kiswahili<br>ii)Uhusiano wa Kiswahili na lugha za kibantu kama kinyarwanda na nyinginezo<br>iii)matumizi na ueneaji wa kiswahili | Mwanafunzi aweze<br>-Kueleza asili ya lugha ya Kiswahili<br>-kutaja uhusiano uliopo kati ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu<br>- Kueleza jinsi lugha ya Kiswahili ilivyoenea Afrika ya mashariki na kati |
| | | |

## KIDATO CHA SITA

| MADA KUU | MADA NDOGO | MADHUMUNI MAHUSUSI ( mambo ya kuzingatia) |
|---|---|---|
| **1.UAMBISHAJI NA MYAMBULIKO WA MANENO** | **i-**Vitenzi<br>ii-viambishi<br>iii-viambishi awali<br>iv viambishi kati<br>v- viambishio tamati<br><br>Mfano[: <u>Analima</u><br>A –Kiambiashai awali kinachowakilisha <u>Kitenzi</u><br>NA-Kiambishi awali mfuatano kinachowakilisha <u>wakati</u><br><br>LIM – Mzizi aushi | -Mwanafunzi weze kueleza maana ya kiambishi<br>-Kutaja aina mbalimbali za viambishai<br>- Kutofautisha viambishi katika vitenzi |

| | | |
|---|---|---|
| | ( kiambishi kati)<br>A- Kiambishi tamati kinachoonyesha ukamilisho wa tendo<br><br>iii)Unyambulishaji wa vitezi<br><br>a) Maana ya unyambulishaji<br>mfano :-lima<br>-limiana<br>-limisha<br>-limishwa<br>-limishana n.k<br><br>b) cheza<br>-chezea<br>-chezewa | Mwanafunzi aweze<br><br>-Kunyambulisha vitenzi mbalimbali<br><br>- kueleza neno kunyambulisha |

| | | |
|---|---|---|
| | -chezeana<br>-chezesha<br>-chezeshana | |
| **2.FASIHI ANDISHI** | i)Tofauti zilizopo kati ya tamthiliya na riwaya<br><br>ii)uchambuzi wa vitabu vya :<br>a) Riwaya ( hadithi ndefu)<br>b) Tamthiliya<br><br>Uchambuzi wa vitabu vya fasihi huzingatia vijengavyo :<br><br>i) <u>Fani</u><br>mfano<br>-wahusika | Mwanafunzi aweze<br>-kutofautisha kati tamthiliya na riwaya<br>Kujua riwaya ,tamthiliya ushairi, kama uwanja wa fasihi simulizi<br><br><br><br><br>Mwanafunzi aweze: |

| | | |
|---|---|---|
| | -mtindo<br>-muundo<br>-lugha n.k<br>ii) <u>Maudhui</u><br>- Lengo la mwandishi<br>- Dhamira (wazo kuu)<br>- Ujumbe<br>- Kufanikiwa au kutofanikiwa kwa mwandishi<br><br>C) <u>Ushairi</u><br>-Maana ya ushairi<br>i) <u>Fani</u><br>-muundo<br>-lugha<br>-mtindo | -Kuchambua ka**zi** ya sanaa akizingatia <u>Fani</u> na <u>maudhui</u><br><br>Mwanafunzi aweze<br>-Kujua maana ya ushairi<br>- kutaja aina mbalimbali za ushairi<br>-Kuchambua Fani na maudhui yaliyomo kati ushairi<br><br>Mwanafunzi aweze<br>Kutaja mifano mbali mbali |

| | | |
|---|---|---|
| **3.HISTORIA YA KISWAHILI**<br><br>( utohowaji wa maneno**)** | Uhusiano wa lugha ya Kiswahili na lugha za kigeni kama:<br><br>i)Kiarabu — Kiswahili<br><br>Swalah — Sala<br>Khabar — Habari<br><br>ii)Kireno — Kireno<br><br>Mesa — Meza<br><br>iii) Kihindi — Kiswahili<br>Paisa — Pesa<br><br>iv)Kijerumani — Kiswahili<br><br>Schule — Shule | misamiati ya Kiswahili iliyotokana na lugha za kigeni |

| | | |
|---|---|---|
| | Kiingereza Kiswahili<br><br>Bicycle Baiskeli<br>n,k | |
| **UTUNGAJI** | i) Insha<br>ii)Hotuba<br>iii)Risala<br>iv)Simu ya maneno<br>v)Matangazo ilani<br>vi) Taarifa | Mwanafunzi aweze;<br>-Kutambua aina mbalimbali za utungaji<br><br>Kutofautisha miundo |

| | | |
|---|---|---|
| **5.SARUFI(MIUNDO)** | Kupambanua/ kuchanganua tungo:<br><br>a) Njia ya matawi<br>b) Njia ya visanduku<br>c) Njia ya maneno<br>Njia hizo 3 (tatu) zifundishwe na kueleweka msisitizo katika kidato cha sita | Mwanafunzi aweze:<br>Kupambanua tungo kwa kutumia njia zilizopendekezwa |

## NJIA ZA UFUNDISHAJI

Kiswahili ni lugha yenye asili ya lugha za kibantu ,hivyo ni lugha ambayo inaweza kueleweka upesi ikifundishwa vizuri kwa vile wanafunzi wamezoea kuisikia ingawaje haielewi.Ni lugha iliyo na upatanisho wa kisarufi ulio karibu na lugha ya Kinyarwanda

| Mfano | Kiswahili | Kinyarwanda |
| --- | --- | --- |
| | Shati | Shati |
| | Mtoto analia | umwana ararira |

Njia za ufundishaji wa somo hili ni nyingi sana kulingana na fani inayofundishwa lakini kuna njia ambayo inaweza kujumuisha fani zote( Structro -Global Methods). Kwa mfano mwalimu akiwa anafundisha ufahamu wakati huo anaweza kufundisha MSAMIATI ,METHALI, NAHAU n.k. Hata hivyo kuna njia mahsusi ambazo Mwalimu anaweza kutumia anapofundisha nyanja tofauti za lugha , hususani sarufi ambazo ndizo nyanja kuu za lugha yoyote ile.

Ili kurahisishia Mwalimu na kumwonyesha jinsi anavyoweza kulikabili na kulifanikisha somo lake somo, hapa tumeonyesha mbinu mbalimbali za ufundishaji wa lugha hii:

## MAZUNGUMZO

Zoezi la mazungumzo linalenga kumpa uwezo mwanafunzi kutumia lugha ya Kiswahili kwa ufasaha katika somo lake.

Mwalimu hana budi kuzingatia kufundisha kuanzia mambo mepesi wanayoelewa kuelekea wasiyoyajua .Mazungumzo yatakayotolewa darasani yawe yale yenye manufaa kwao, mfano maamkizi,kucheza mpira , usafi n.k.

Inampasa Mwalimu awe Mdadisi kwa kushirikisha wanafunzi wote darasani akitumia mbinu ya majibizano ya wanafunzi wao kwa wao.

Mwalimu akosoe makosa yanayojitokeza kila mara mathalani matamshi , lafudhi, shadda, au kiimbo. Mwalimu awaelekeze namna ya kutambua na kupanga mawazo makuu ya habari aliyoisoma au kusimulia. Mwalimu awaonyeshe mbinu za kujibu maswali yatokanayo na ufahamu.

## MSAMIATI

Katika ufundishaji wa msamiati, mwalimu aeleze maana ya maneno kwa kutumia vitu halisi, picha , maigizo, maswaili na majibu na mifano mbalimbali. Wanafunzi washirikishwe kikamilifu kwa kutoa mifano yao wenyewe.

## UTUNGAJI

Utungaji unaweza kuzingatia fani mbili yaani mazungumzo na kuandika . Mazungumzo yawe juu ya jambo lenye maarifa na manufaa. Mfano ;Umoja na Mshikamano wa Wanyarwanda,amani, maendeleo ya nchi, na magonjwa kama ukimwi n.k.

a) Yawepo matayarisho juu ya jambo litakalozungumzwa ili wakati usipotee bure . Lengo lijulikane wazi tangu mwanzo wa somo.

b) Mwalimu atilie mkazo uchaguzi wa maneno bora na matokeo yake kwenye matumizi.

c) Wanafunzi wapewe mazoezi wakitunga hotuba fupi fupi. Hii inaweza kukuza vipaji vya kujieleza na kujiamini.

d) Mazungumzo na mijadala itumiwe kama chanzo au utangulizi wa kuandika utungaji.

Utungaji wa kuandika unalenga kumwezasha mwanafunzi kutumia lugha hii katika fani na njia mbalimbali katika fani hii kwa ufasaha .Utungaji uanzie kwa mambo mepesi wanafunzi wanayoyafahamu , mfano insha fupi fupi kahusutaratibu za kila siku , michezo ya kuigiza n.k,Mwalimu awaelekeze namna ya kupangilia mawazo kwa utaratibu unaostahili.mmoja mmoja au kwa makundi.

Mazungumzo yanaweza kuambatana na mijadala ambayo yaweza kufanyika aidha ndani au nje ya darasa kulingana na mada inayozungumziwa .Wakati wote mwalimu azingatie kiimbo.( lafudh shadda ), mpango wa mawazo ., matumizi ya semi , nahau na ufasaha wa lugha , ukweli , usawa na uhakika wa mambo .

Wanafunzi wakishapata msamiati wa kutosha Mwalimu hana budi awape nafasi ya kujieleza mbele ya darasa katika kikundi .Hivyo matayarisho kamili yafanyike na

lengo lake liwe wazi. Kazi zinazoweza kufanyika katika somo hili ni kama vile hotuba fupi , michezo mifupi ya kuigiza , hadithi fupi za fasihi simulizi, nyimbo mashairi mepesi, midahalo .

## KUANDIKA

Taaluma ya kuandika haina budi itolewe kwa wanafunzi kuanzia mambo wanayofahamu.Hapa mwalimu inampasa kufuatilia hati ya kila mwanafunzi kuumbo neno, sentensi na vifungu vya habari.Mwalimu hana budi kufuatilia matumizi ya alama na vituo katika hati ya mwanafunzi.Mwalimu atoe mazoezi mengi yaliyo na vipashio visivyopatikana katika lugha ya Kinyarwanda , mfano: dhalimu , thamani, aghalabu n.k

## KUSOMA NA UFAHAMU

Kusoma kwa kutafakari ndilo lengo kuu katika fani hii .Taratibu za kusoma kifungu cha habari zifuatwe, mathalani kusoma kimya kimya,kwa sauti na kwa haraka .Mwaslimu anaweza kumtumia mwanafunzi mmoja kusoma huku wengine wakifuatilia vitabuni mwao.

## KUSIKILIZA

Mwalimu atumie vipengele mbalimbali katika kuzoeza usikivu wa wanafunzi wake, katika mazungumzo, hadith , nyimbo na ushairi.

Vitu hivyo vinaweza kuwa ni moja kwa moja au vilivyonaswa kwenye kanda za sauti , kama baada ya kupewa kichwa cha habari ya kuzungumzia kikundi kimoja cha wanafunzi kinaweza kupewa fursa ya kuzungumza .

Wanafunzi wengine watasikiliza na baadaye kutoa mhutasari wa yaliyozungumziwa au kutoa yanayohusu mazungumzo hayo.

Hali kadhalika vifungu vya habari , hadithi nyimbo na mashairi vinaweza kutumika katika kupima matamshi ambayo labda bado yanaathiri uzungumzaji wa wanafunzi. Wakati mwingine itambidi Mwalimu apange zoezi maalum kama kusoma au kuimba kifungu cha maandishi chenye kukazia sauti fulani inayokosewa na wanafunzi.

N.B stadi ya usikivu hufundishwa pamoja na stadi nyingine ili kupumzisha mara kwa mara akili ya mwanafunzi, kama kuimba ,kutoa mhutasari wa yaliyosikilizwa , chemsha bongo n.k

## UFUNDISHAJI METHALI NA VITENDAWILI

Methali hutumia lugha ya mkato yenye kubeba shehena kubwa ya maudhui na ujumbe , katika methali kuna mafunzo , maonyo na marekebisho mbalimbali ya maisha ya jamii.

Aghalabu methali hutumia lugha ya mafumbo ambayo huhitaji kufumbuliwa ili kuweza kunufaika na maadili yaliyofichwa ndani ya methali inayohusika .

Walimu wanaofundisha kiswahili wanapaswa kufundisha methali kama wanavyofundisha maandishi mengine ya Fasihi.

Watachambua maudhui yaliyomo katika kila methali , maana yake, ujumbe uliomo katika methali , mafumndisho yaliyomo katika methali na matumizi ya methali hiyo.
Mfano``**MVUMILIVU HULA MBIVU**`` Maana ya methali hii ni kwamba asiwe mtu mwenye kukata tamaa upesi, maudhui yanayojitokeza katika methali hii ni kwamba kila kitu kizuri hupatikana kwa shida na ili mtu akipate hupaswa kuambatana na matatizo mengi.

Ujumbe tunaopata katika methali hiyo ni kwamba ili mtu afanikiwe katika jambo fulani hana budi kukabiliana na matatizo yote bila kukata tamaa.

Mwalimu wa Kiswahili anapaswa kufundisha methali kwa kueleza maana ya methali yenyewe, maudhui yaliyomo katika methali , ujumbe na mazingira ya methali hiyo .

Vitendawili pia vina maudhui , maadili na ujumbe ndani yake.Vitendawili ni semi fupifupi zilizo fumbwa ambazo mtu anapaswa kuzifumbua ili kupata manufaa yaliyomo katika kitendawili hicho .

Mfano

## NJIA ZA KUFUNDISHA MASHAIRI, TENZI, NA NGONJERA

Mashairi, Tenzi na Ngonjera ni fani mojawapo maarufu katika fasihi iliyobeba shehena kubwa ya maadili na ujumbe ndani yake.Wakati wa kufundisha mashairi, ngonjera na Tenzi mwalimu hana budi kusoma kwa uangalifu ubeti hadi ubeti ili kupata maudhui, maadili na ujumbe uiotolewa na wasanii katika sanaa waziandikazo. Mfano katika kuchambua mashairi, njia zifuatazo zinaweza kutumika :

Kwanza ni kuchunguza maudhui yaliyomo katika shairi kama yanazungumzia masuala ya kisiasa, kiuchumi , kiutamaduni au yale ya kijamii.

Pili ni kuchambua ubeti kwa ubeti kwa kilamstari au utenzi ili kupata dhana iliyomo katika kila ubeti.
Tatu ni kuchunguza maudhui , maadili na ujumbe uliomo katika kila shairi.Mwalimu akifanya hivyo atawezesha wanafunzi kupata maadili na ujumbe katika mashairi wayasomayo, na hii itawasaidia wanafunzi kuona migogoro na matatizo yaliyomo katika jamii na jinsi ya kutatua migogoro hiyo.

Vilevile katika ufundishaji wa vipengele hivyo , fani na maudhui vionyeshwe wazi kwa wanafunzi, na kuambiwa kuwa ni vitu muhimu ambavyo haviachani.

Katika ufundishaji wa fani mwalimu hana budi kuangalia mbinu na taratibu za utungaji wa mashairi. Mfano:Mashairi ya kimapokeo:Mwalimu awaeleze wanafunzi miundo mbalimbali iliyotumika hasa Mashairi upande wa fani.

-Yafanyike majadiliano kuhusu mahusiano kati ya hadithi na hali halisi ya maisha .
-Yachunguzwe maadili / mafunzo yaliyomo
-Falsafa ya mwandishi/ msimamo wa hadithi
-Hadithi inamhusu nani? Jamii ipi na kwa vipi ?

Mwalimu yampasa kupitia kipengele cha mtazamo wa fikra .

Mtazamo wa fikra huonyesha jinsi mtu anavyotazama au kufafanua kile kinachomgusa au kinachomchomachoma moyoni mwake .Katika ushairi viungo vya mwili vinaweza kupewa utu, nafsi na uhuru wa kuishi kama viumbe vyenye nafsi za pekee vinavyoweza kufikiri na kuamua vyenyewe .

Katika ulimwengu wa ushairi miti , wanyama , jua , mwezi na vitu vyote vionekanavyo juu ya uso wa dunia vyaweza kupewa uhai na utu vikaishi kama binadamu.

Jina la kitabu lijadiliwe na kulinganishwa na maudhui yake .Udhaifu na usanifu ujadiliwe.
Mwanafunzi apewe fursa ya kutoa maoni juu ufundi uliotumika katika andiko/ hadithi na pawepo mijadala ya wanafunzi kuhusiana na migogoro iliyomo na usuluhishi wake.

**NJIA ZA KUFUNDISHA FASIHI**

Ziko njia nyingi ambazo mwalimu wa somo la fasihi anaweza kuzitumia ili kufanikisha somo lake na kuwafanya wanafunzi kulipenda somo la fasihi lakini hapa zimependekezwa njia zifuatazo:

Njia ya kwanza ni njia ya majadiliano ya darasa zima.Njia hii huweza kuwasaidia wanafunzi kujenga staidi ya kuzungumza.
Huwazoeza wanafunzi kusema na kujadili mambo mbalimbali mbele ya hadhara bila woga . Njia hii si kwamba inawazoeza kuzungumza hadharani tu bali inawafunza namna yakujadili mambo yenye mantiki.
Pia hupevuka kimawazo na kuweza kujadili mambo kwa undani zaidi.

Njia ya pili ni ile ya vikundi vya majadiliano wanafunzi hugawanywa katika vikundi vidogo vidogo vyenye washiriki watano hadi saba . Baada kuligawa darasa katika vikundi, Mwalimu hutoa swali moja kwa kila kikundi, ili kila kikundi kijadili swali lake kwa uwezo wake.Njia hii huwapa nafasi wanafunzi wengi katika kikundi kutoa mawazo mbele ya kikundi bila haya .

Njia ya tatu Mwalimu anaweza kutumia njia ya mazoezi. Kawaida katika njia hii Mwalimu hutoa maswali kadhaa kufuatia njia iliyokwisha fundishwa .Maswali yaweza kufanyiwa humo darasani katika kipindi cha somo la fasihi.

Mwisho Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kutafuta fani na maudhui katika kuchambua au kuhahakiki vitabu mbalimbali vya fasihi.

## NJIA ZA KUFUNDISHA HADITHI

Mwalimu afundishe somo hili kwa kutumia vipengele vifuatavyo:

i) Wanafunzi wasome na kuelewa yaliyomo katika hadithi na kisha majadiliano na mazungumzo yafuate.

ii) Maoni juu ya hadithi hiyo yatolewe kuhusu aina au lengo lake pamoja na mazingira yaliyotumwa katika hadithi.

iii) Mwalimu aonyeshe muundo,mawazo hadi mwisho wa hadithi, mtiririko wa visa , mahali palipo na upeo wa hadithi , aonyeshe jinsi muundo unavyosaidia katika kuelewa hadithi na mtiririko wa masimulizi.

iv) Mwalimu afundishe dhamira , wazo au ujumbe ulioko katika hadithi, baada ya kusikiliza mchango wa wanafunzi kuusiana na hoja hiyo.

v) Wahusika wajadiliwe na uhusika wao.Mjadala ufanyike kuhusiana na vipengele vya maswali.

Mfano: - nani mhusika mkuu

-Wahusika wanahusiana je wao kwawao

- Ni zipi nafasi zao katika hadithi

- Wamepevuka vipi lengo na dhamira ya mwandishi.

Kipengele cha mtindo katika ufundishaji wa hadithi kielezwe na kujadili maswali.

Mfano:-Nani anasimulia ? na kwa ninin ?

- Mwandishi ametumia mbinu gani katika kuwasilisha mawazo yake ?
- Matumizi ya picha , lugha na vipengele vyake

**TATHMINI**

Kwa kila kazi yoyote inayotolewa darasani haina budi kufanyiwa tathmini ili kujua uelewa wa wanafunzi.Hii humsaidia Mwalimu kuelewa pamoja na kumwezesha kuendelea na somo anaporudia somo hilo.Mwalimu inambidi ajue sababu za kutofanikiwa kwa somo lake na ikibidi aweze akabadili njia za ufundishaji.

Katika kutathmini mwalimu anashauriwa yafuatayo:
-Kutoa zoezi kila baada ya somo na masahihisho yafanywe kabla ya kuendelea na somo jingine .

Mwalimu anashauriwa kutumia maswali ya mdomo akiwashirikisha wanafunzi ili wajenge tabia ya kujieleza na kujiamini.

-Mazoezi ya takayotolewa yazingatie stadi za kusoma , kuandika na kuzungumza .
-Katika kufanya tathmini Mwalimu anashauriwa kutumia aina mbalimbali za utunzi wa maswali.

Mfano : i) Maswali kujibu kweli au si kweli.
ii)Kutaja
iii)Kuoanisha
iv)Kujaza nafasi zilizo wazi.
v)Maswali ya kujieleza , kujadili n.k

-Mwalimu atoe mazoezi ya kufanyia nyumbani na masahihisho yafanyike kabla ya kuendelea na somo linalofuata .
-Kila baada ya kumaliza mada mwalimu anashauriwa kutoa jaribio kwa wanafunzi ili kupima uelewa wao, ieleweke pia kuwa majaribio baada ya mada hazimzuii mwalimu kutoa majaribio ya dharura ili kuona iwapo wanafunzi hufuata somo hili.

Mtihani ni lazima utolewe kila baada ya kumaliza muhula . Maswali yatokane na mada zote Zilizofundishwa katika kipindi hicho, lakini hii haimzuii Mwalimu kutumia baadhi ya Maswali kutoka vidato vilivyotangulia ili kupima kumbukumbu ya wanafunzi.

Tathmini itolewe kila baada ya muhula wa mwisho . Mtihani ni lazima uhusishe mada zote zinazofundishwa kwa mwaka mzima . Vile vile hii haimziuii Mwalimu

kutoa maswali yanayotokana na ujuzi wa jumla bila kuangalia ya kwamba mwanafunzi alifundishwa au la.

## MAPENDEKEZO

Ili kufanikisha madhumuni ya mhutasari huu , mambo yafuatayo yamependekezwa:

1. Walimu watakaofundisha somo hili wapewe Semina za kutosha kuhusiana na ufundishaji wa mada zilizo katika somo hili.

2. Ili kuendeleza lugha hii nchini Rwanda , wizara haina budi kuwa na ushirikiano na Taasisi za ukuzaji wa lugha ya Kiswahili zilizoko katikanchi jirani zenye uzoefu na taaluma ya kutosha katika ufundishaji na utaratibu wa lugha hii ya Kiswahili. Mfano BAKITA ( Tanzania), vile vile Kenya na idara za ukuzaji wa lugha za Kiafrika na Ulimwengu.

3..Katika uimarishaji wa Kiswahili,inapendekezwa kuundwe chombo maalum cha kitaifa kitakachoshughulikia lugha hii yaani uratibu na uenezaji wa lugha hii

4.Walimu wapewe motisha kila inapowezekana ili kuleta hamasa katika utendaji wao wa kazi.

5.Washirikishwe wataalamu wachache waliopo katika kutunga vitabu,majarida na vitini vitakavyosaidia katika ufundishaji wa somo hili.

6. Vitabu, majarida yanayoeleza kuhusu matatizo yanayoikumba jamii vitungwe au kuandikwa hasa vile vinavyohusu na kujilinda na magonjwa ya hatari kama vile ukimwi yaani (sida )

7.Kuwepo ukaguzi wa mara kwa mara katika shule ili kuona jinsi gani Somo la Kiswahili linavyofundishwa.

8. Kuwepo chombo cha kitaifa cha kushughulikia mitihani kwa ngazi ya taifa ( Baraza la Mitihani)

10.Vitabu visivyopungua viwili kwa kila fani ya fasihi yaani Riwaya, tamthiliya na ushairivifundhwe na ushairi vifundishwe

VITABU VYA FASIHI VILIVYOPENDEKEZWA

A.RIWAYA

| | |
|---|---|
| 1.Nyota ya Huzuni | George Lewanga |
| 2.Ndoto ya Ndaria | John Ngono |
| 3.Adili na Nduguze Macmillian and co LTD London 1966 | Shabaan Robert |
| 4.Kuli | Shafi Adam Shaf |

B TAMTHILIYA / MICHEZO YA KUIGIZA

| | |
|---|---|
| 1.Wakati Ukuta East African Publication House 1996 | Ibrahim Hussein |
| 2.Hawala ya Fedha | Amandina Lihamba |
| 3. Kijiji chetu | Ngalimecha Ngalihyoma |
| 4. Njia Panda | Mhanika |

## C USHAIRI

| | |
|---|---|
| 1.Diwani ya Mnyampala East African Publishing Arusha , Dar-es- salaam 1998 | Mathias Mnyampala |
| 2.Diwani ya Akili ,East African Literature Bureau, Nairobi, 1975 | K.H.A na Snow white |
| 3.Mashairi yetu, East African Publishing House Nairobi 1981 | M.K Khan |

## D VITABU VYA REJEA

| | |
|---|---|
| 1.Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo Tanzania Tanzania Publishing House Dar-es-Salaam 1978 | F.M.V NKWERA |
| 2. Mafunzo ya Kiswahili Longman, Nairobi 1975 | M.Kamal Knan na Yahya |
| | |

| | |
|---|---|
| 3.Sarufi Maumbo ya Kiswahili Kitabu cha Kwanza ,<br>Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Sanifu,<br>Chuo Kikuu Dar-es –Salaam 1997 | C. Kapinga |
| 4.Majina / Nomino za Kiswahili, (MAKALA) Taasisi ya Elimu Kigali , 1980 | P.M. Ntumbo |
| 5. Historia ya Kiswahili , Oxford University Press, Nairobi, 1980 | Shihabuddin Chiraghdin na Mathias Mnyampala |
| 6.Insha na Mashairi, Mzalendo Publishers Nairobi | B.N. MAGARI |
| 7. Darasa za Kiswahili Kitabu cha I&II Oxford University Press Nairobi press 1980 | Shihabuddin Ghiradin |
| 8.-Kitabu cha kiswahili I<br>Kitabu cha mwanafunzi<br><br>- Kitabu cha kiswahili IV-VA | Taasisi ya mafunzo sekondari 1986 |

| | |
|---|---|
| Kitabucha mwanafunzi<br><br>-Kitabu cha Kiswahili<br>IV-VC<br>Mafunzo ya Uongozi na Sheria<br><br><br>-Kitabu cha Kiswahili II<br>Kitabu cha mwanafunzi | - do-<br>novemba1987<br><br><br>-do-<br>novemba 1987<br><br>Bureau pedagogique de l`enseignement Secondaire<br>Janvier 1984 |